

Ukweli Wa Injili

MAFUNDISHO YA BIBLIA NA HIMIZO KWA
KAZI YA KIMISHENI ULMWENGUNI KOTE

HABARI NJEMA YA INJILI

Mwangaza mkuu ulipensa usiku uliokuwa na giza nyingi, nao halaiki kubwa ya malaika wakajaza anga lote. Kwaya hiyo ya mbinguni ikatoa sauti ya wimbo ulioambatana vizuri, wimbo wa kumsifu Mwenyezi Mungu. Malaika hao wakatangaza kwa ujasiri na furaha kuu: "Atukuzwe Mungu juu mbinguni, na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia" (Luka 2:14).

Kama wewe ungalikuwa pale miaka elfu mbili iliyopita na kutazama na kupata ujuzi wa jambo hilo la ajabu wadhani ungalihisi vipi? Je, ni nini kilisababisha watumishi hawa wa Mungu kuja duniani kuleta ujumbe wa amani na mambo mema kwa wanadamu? Sababu yake ilikuwa ni kule kuzaliwa kwa Yesu Kristo mwana wa Mungu aliye hai.

Miaka 30 baadaye wakati Yohana Mbaitaji alimwona Yesu alisema, "Tazama, Mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwenguni!" Basi si jambo la kushangaza kwamba malaika walifurahishwa sana na kuja kwa Masiya ambaye angewakomboa wanadamu na



*"Kama vile maji ya baridi
kwa mtu mwenye kiu,
ndivyo ilivyo habari njema
itokayo katika nchi ya
mbali."*

Mithali 25:25

kuvunja nguvu za dhambi na kifo maishani mwa wanadamu.

Dhambi imejaa ulimwenguni na inaleta majonzi mengi na hali ya watu kujihisi kuhukumiwa, upweke, kifungo, na watu kukata tamaa. Maisha ya watu na ya familia inaangamizwa kuititia kwa nguvu za Shetani. Lakini kuititia kwa

nguvu za Yesu Kristo kungali kuna tumaini kwa ajili ya mwanadamu hata wakati huu kwenye ulimwengu ulioaja shida nyingi. Kupitia kwa Yesu Kristo nguvu za dhambi zinaweza kuvunjawavunjwa na hali ya tumaini na uhai ikaweza kuweko badala ya hali ya kuvunjika moyo na kifo.

Mithali 25:25 inasema "Kama vile maji ya baridi kwa mtu mwenye kiu, ndivyo ilivyo habari njema itokayo katika nchi ya mbali." Mtu hupata nguvu mpya anapopata habari njema wakati ambapo hapo mbeleni aligandamizwa na mambo na kuwa na matatizo chungu nzima. Kuna habari njema kwa kila nafsi inayosumbuka. Habari hizo zinapatikana katika Yesu Kristo. Maana ya injili ni "habari njema" ama "taarifa ya kufurahisha." Habari njema za injili ni kwamba Yesu Kristo alikuja kutufanya kile ambacho hatungeweza kujifanya. Yesu Kristo angali anafanya miujiza maishani mwa watu kwa kuwaponya na kuwarudishia wote ambao ni wagonjwa

(Inaendelea kutoka ukurasa 2)

MAMBO YENYE BIBLIA

Inafundisha Kuhusu...

Neno la Mungu

2 Tim. 3:6, 2 Petro 1:20-21, Mat. 24:35

Uhusiano wa Upendo

Mat. 22:37-40, Yohana 14:21-23,
1 Yohana 4:7-21

Toba

Matendo 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10

Uzao Mpya

Yohana 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rumi 6:1-4,
Efeso 2:1, 5-6

Uhuru Mbali na Dhambi

1 Yohana 5:18, Mat. 1:21, Yohana 8:11.

Ujazo wa Roho Mtakatifu

Matendo 19:2, 15:8-9, 1:8

Utakatifu

Lk. 1:73-75, Waebrania 12:14, 1 Petro
1:15-16, Tito 2:11-12, Rumi 6:22

Ufalme wa Mungu

Luk. 17:20-21, Rumi 14:17,
Yohana 18:36

Kanisa

Matendo 2:47, Efeso 4:4-6,
1 Kor. 12:12-13, Kol. 1:18

Umoja

Yohana 17:20-23, Wagaltia 3:28,
Ufunuo 18:2-4.

Kumbukumbu

Mat. 28:19-20, 26:26-30,
1 Kor. 11:23-27, Yohana 13:14-17

Uponyaji wa Kiungu

Lk. 4:18, Isaya 53:4-5, Yakobo 5:13-16

Utakatifu wa Ndoa

Mat. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3,
1 Kor. 7:10-11.

Mavazi ya Nje

I Tim. 2:9-10, I Kor. 11:14-15,
K. Torati. 22:5

Mwisho wa Nyakati

2 Petro 3:7-12, Yohana 5:28-29,
2 Kor. 5:10, Mat. 25:31-46

Kutojipigania

Lk. 6:27-29, 18:20

Ibada

Yohana 4:23-24, Efeso 5:19, 2 Kor. 3:17

Mwito Mkuu

Marko 16:15

(Endelea kutoka ukurasa I)

wa kiroho hali bora ya maisha. Yesu atafanya njia mahali ambapo hamna njia. Yesu atafanya kisichowezekana kiwezekane.

Ujumbe wa mwanzo kabisa ambaeo Yesu alihubiri ulifafanua habari njema za injili: "Roho wa Bwana yu juu yangu, Kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema. Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, na vipofu kupata kuona tena, kuwaacha huru waliosetwa, na kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa" (Luka 4:18-19).

Yesu anakupenda na habari njema za injili yake zingali zinafanya kazi hadi leo. Yeye angali kwenye shughuli ya kumsamehe mwenye dhambi na kuponya wagonjwa. Yesu atamhudumia kila mtu ambaye hana fura, mwenye maumivu, kipofu, na mwenye majeraha. Kile ambacho wewe unahitaji kufanya ni kufungua moyo wako na kumlilia Bwana. Yeye anasikia kilio chako.

"Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbbe" (Marko 16:15). Injili hii ya tumaini na ambayo ina utukufu mwingu ni kwa ajili ya watu wa tabaka zote, watu wa aina zote, na watu wa kila taifa. Kwa kiwango ambacho tutapata ujuzi wa habari njema hebu tuendelee kuwa waaminifu kuishiriki na wale wote ambaeo wametuzunguka na ambaeo wana maumivu. Habari njema hailingani na kile ambacho tunaweza kufanya bali ni yale ambayo Yesu anawenza kufanya, na kwa kweli kile ambacho atakifanya. Utukufu wote uwe kwake Mungu kwa sababu ya habari njema ya injili. ■

UKWELI WA INJILI

Gazeti la Ukweli wa Injili huchapishwa kwa jina la Bwana kwa ajili ya watu wote wa mataifa yote kwa kusudi la kuwapatia msingi bora na kuwahimiza watu wa Mungu kupitia kwa ukweli wa Neno la Mungu. Gazeti hili hufunzo na kupigia debe kweli za Biblia ambazo zimekuwako tangu wakati wa Yesu na mitume. Neno la Mungu ndilo msingi wa pekee wa imani ambayo inakubalika na ambayo sisi tunaamini. Neno hilo linafundisha kuhusu wokovu na ukombozi kutoka dhambini kupitia kwa utakaso wa Yesu Kristo; na hapo baadaye mtu hujazwa Roho Mtakatifu ili amwongoze, amuonyeshe njia, na pia kumpatia nguvu. Wokovu huo pia unahuishi mtu kuwa na utakatifu wa vitendo katika kila fani ya maisha yake; na pia kuhusisha umoja na ushikamano wa watu wa Mungu. Huduma ya Mungu ambayo inakubalika ni kwa mtu kuwa na uhusiano wa kibinasi na Yeye, uhusiano ambaeo ni wa upendo na ambaeo msingi wake ni ukweli.

Wahariri: Michael na Rene Smith

JIANDIKISHE ILI UPATE NAKALA YAKO

Ukweli wa Injili ni gazeti la kielektroniki ambalo litachapishwa kulingana na mwongozo wa Bwana. Tutembelee katika tovuti yetu ya www.thegospeltruth.org ili ujandikishe kupata notisi ya kupokea nakala zitakazokuwa zilkipapishwa. Hebu jisikie huru kutumia mhariri wa gazeti hili orodha ya majina na anwani pepe za wale ambaeo wangependa kupokea toleo hili.

ANWANI

Ukweli wa Injili huchapishwa katika nchi tofauti tofauti ili isambazwe katika nchi hizo. Yeote ambaye anataka kuunga kazi hii mkono anawenza kutuma msaada wake kupitia kwa ofisi hii. Kazi hii na zingine za kimisheni ambazo zinafanya na ofisi hii zinaungwa mkono na matoleo ya hiari ambayo hutolewa kwa jina la Kanisa la Mungu. Ukita-ka unawenza kuomba upewa risiti kulingana na jinsi tumelipa ushuru kutokana na matoleo yako ya kifedha.

UKWELI WA INJILI, 605 Bishops Ct., Nixa, MO 65714 USA

editor@thegospeltruth.org

Tahariri



Lakini ikiwa injili yetu imesitirika, imesitirika kwa hao wanaopotea; ambao ndani yao mungu wa dunia hii amepofusha fikira zao wasioamini, isiwazukie nuru ya injili ya utukufu wake Kristo aliye sura yake Mungu. Kwa maana hatujihubiri wenyewe, bali Kristo Yesu ya kuwa ni Bwana; na sisi wenyewe kuwa tu watumishi wenu kwa ajili ya Yesu. —2 Kor. 4:3-5

Sisi tunaishi katika kizazi ambacho kimepofushwa, sio tu na tamaa za mwili, bali pia na idara za dini. Ni ombi langu kwamba kila mtu ulimwenguni huu angeweza kuja na kupata ujuzi wa imani ya kweli ambayo inapatikana katika Yesu Kristo. Mhubiri yeyote au kanisa ambalo ‘linajihubiri lenyewe’ ni mhubiri au kanisa la uwongo. Kwa kweli katika nguvu na uwezo wetu hatuna chochote cha kupatia ulimwengu uliopotea. Sisi tuna uwezo tu wa kuwaelekeza watu kwa Mwokozi – sio tu kwa maneno yetu, bali pia kwa mwangaza ambao unatoka ndani yetu kutokana na Kristo ambaye anaishi ndani yetu.

Ni shauku langu kwamba mwangaza huu wa injili ambayo ina utukufu uendelee kung’aa hata zaidi katika siku hizi ambazo zina giza na uovu. Katika huduma ya miaka mingi ambaye nimefanya kote ulimwenguni nimetambua kuna haja kubwa ya kusaidia uanzilishaji wa huduma za kimsingi katika ukweli wa neno. Kusudi letu sio kupata wafuasi au kumfanya mtu fulani ‘kujiunga’ na kikundi fulani. Lengo letu ni kufunza na kuwashimiza watu kujiunga na Kanisa lolote ambalo linapatikana katika mahali walipo. Kwa njia hiyo umoja unapatikana wakati watu wanafuata ukweli huku wakiongozwa na Roho.

Miezi kadhaa iliyopita katika nchi ya Kenya (kufuatia mahubiri ya ujumbe rahisi wa injili) mhudumu mmoja wa kanisa la mahali hapo akaniambia, “Ujumbe wako ulikuwa wa kutia moyo sana.” Baadaye yeye akaniambia kwamba wahudumu wengi wanaokuja kuwashudumia huja ili kujenga jina lao wenyewe. Lakini hamna uhuru wa kweli ambao hupatikana kwa kumfuata mtu au dini fulani. Kwa kweli mimi najihisi kuchoshwa sana na dini na umwili ambao hupatikana kati ya watu ambao huijita Wakristo. Kwa sasa mimi natangaza wazi wazi upendo wangu kwa Mungu, upendo wa ukweli, na pia ninawapenda watoto wote wa Mungu. Moyo wangu umejaa machozi kwa ajili ya mwenye dhambi, kwa ajili ya manafiki, na kwa ajili ya waliorudi nyuma, ili wote wapate utoshelevu wa kweli. Kutosheleka huko hakupatikani katika kuta nne za kanisa wala hakupatikana kwa mtu kufuata njia bora za dini. Kutosheleka huko hakupatikana kwa mtu kupata ujuzi (wa kujitolea mhanga) kwa Yesu Kristo na kufuata njia ya Biblia ambayo ni nyembamba, yenye furaha, na ya kujinyima, ambayo ndio humwongoza mtu hadi uzima wa milele.

Ni kusudi langu na la mke wangu kwamba tuweze kushiriki kuititia kwa neno linaloandikwa kwenye gazeti hili baadhi ya kweli za biblia ambazo ni za kimsingi na ambazo zinaweza kuwasaidia watu wanaomtafuta Mungu kwa kweli, ili tuweze kuegemezwu katika ukweli huo.

Sisi tutaendelea kuchapisha gazeti hili mradi tu Bwana ataendelea kutupatia muda na mwongozo. Basi tunawaomba muendelee katuombea ili tuweze kutimiza lengo hili na ili liweze kafaaula katika mambo ya kiroho.

Hebu tumwombe Mungu ili aweze kubariki kila mkutano wetu katika msimu huu. Kwa kweli kungali kuna nguvu katika maombi na mimi natazamia kwamba kuna milima itakayofanywa tambarara kuititia kwa nguvu zake Mungu.

Michael W Smith

mengi kwenye
MTANDAO

Nenda kwa

thegospeltruth.us

kupata jarida jipya.



MAWAIDHA 6 YA MTU ANAPOJIFUNZA BIBLIA

PATA MAHALI PA KUANZIA

Tafuta andiko au kitabu cha Biblia ambacho wataka kujifunza. Kitabu cha Injili, kitabu cha Yakobo, Tito, 1 Petro na 1 Yohana ni vitabu vizuri vya kusomwa na Mkristo mpya.

ANZA NA MAOMBI

Mwombe Mungu akupe hekima, uongozi na uwezo wa kuelewa. Unapoomba kumbuka kwamba maneno ambayo unasoma yamewekwa uhai na Mungu: "Kufafanusha maneno yako kwaitia nuru" (Zaburi 119:130).

SOMA ANDIKO LOTE

Msingi wa mafundisho mengi ambayo si ya kweli hutokana na maandiko kadhaa kuchukuliwa yakiwa peke yake na kunakiliwa nje ya muktadha wake. Soma andiko lote ili upate ukweli wote.

KUWA MAKINI KWA MENGI AMBAYO YAPO KWENYE ANDIKO HILO

Gawanya andiko lote aya baada ya nyininge na ujifunze zaidi ili upate maana ya ndani. Tazama maana ya maneno yaliyotumika humo au maandiko mengine ambayo yanaunga mkono dhana inayopatikana kwenye maandiko hayo. Andika kwenye daftari mambo ambayo unajifunza kutoptana na maandiko hayo.

KANUNI ZA KUFANYISHA MAANDIKO KAZI KAZI KATIKA MAISHA YAKO YA KILA SIKU

Mruhusu Mungu akuzungumzie kibinagsi. Je, andiko hilo linahusiana na maisha yangu kwa njia gani?

"IWENI WATENDAJI WA NENO"

Fanyisha Neno kazi katika maisha yako ya kila siku. "Neno la Kristo na likae kwa wingi ndani yenu katika hekima yote" (Wakolosai 3:16).

MAFUNZO YA BIBLIA

SOMO: UKWELI

Somo la Biblia

Basi Pilato akamwambia, Wewe u mfalme basi? Yesu akajibu, Wewe wasema, kwa kuwa mimi ni mfalme. Mimi nimezaliwa kwa ajili ya haya, na kwa ajili ya haya mimi nalikuja ulimwenguni, ili niishuhudie kweli. Kila aliye wa hiyo kweli hunisikia sauti yangu. Pilato akamwambia, Kweli ni nini? Naye akiisha kusema neno hilo akawatokea Wayahudi tena, akawaambia, Mimi sioni hatia yo yote kwake. —Yohana 18:37-38

Maana ya Neno Ukweli: *kile ambacho kinalingana na ushahidi uliopo; hali ya kuwa na uhakika, usahihi, kusema kweli, yenye kulingana na vipimo vyake, isioya na shaka; hali ya kuwa hivyo; Kwa lugha ya Kiyunani: isiyoficha yaliyo ndani yake.*

I. Yesu ni Ukweli

- A. Yohana 1:14 Neno (Yesu) akafanyaika mwili – huku akijaa neema na ukweli.
- B. Yohana 1:17 Neema na ukweli ulikuja kwa njia ya Yesu.
- C. Yohana 14:6 Yesu ndiye njia, kweli, na uzima.

II. Neno la Mungu ni Ukweli

- A. Yohana 17:17-19 Neno la Mungu ni ukweli.
- B. 2 Timotheo 2:15 Jitahidi kutumia kwa halali neno la kweli.
- C. 2 Wathesalonike 2:10 Inabidi mtu kupenda ukweli ili aokoke.

III. Roho wa Kweli na Ibada

- A. Yohana 16:13 Roho Mtakatifu ataongoza kwa kweli zote.
- B. Yohana 4:22-24 Kuabudu kwa Roho na kwa Kweli.

IV. Ukweli haubadiliki na ni wa Milele

- A. Isaya 40:8 Neno la Mungu litasimama milele.
- B. Zaburi 100:5 Uaminifu utadumu kwa vizazi vyote.
- C. Luka 21:33 Maneno ya Kristo hayatapita kamwe.

V. Faida za Ukweli

- A. Yohana 8:32 Ukweli huweka huru.
- B. Yohana 3:19-21 Ukweli huonyesha na kuleta kwenye mwanga.
- C. 1 Petro 1:22-23 Nafsi zetu hutakaswa kwa sisi kutii ukweli.

VI. Kuachana na Ukweli

- A. 2 Timotheo 4:1-4 Watu watakataa ukweli.
- B. 2 Timotheo 2:16-18 Watu walokosa ukweli.

VII. Waalimu wa Uwongo

- A. 2 Petro 2:1-2 Kutakuwa na waalimu wa uwongo kati yenu.
- B. Mathayo 15:9 Mafundisho yao yatokana na maagizo ya wanadamu.
- C. Tito 1:14 Jiepushe nao.
- D. 1 Timotheo 6:3-5 Tengana na waalimu wa uwongo.

VIII. Adhabu kwa Wale Wasiotii Ukweli

- A. Warumi 2:8-9 Dhiki na shida.
- B. 2 Wathesalonike 1:8 Kulipiza kisasi.

IX. Kanisa

- A. 1 Timotheo 3:15 Nguzo na msingi wa ukweli.
- B. Zekaria 8:3 Sayuni (kanisa) utaitwa mji wa ukweli.

X. Changamoto

- A. Mithali 23:23 Nunua ukweli na usiuuze.
- B. 1 Yohana 1:6 Fanya ukweli kwa kutii amri.
- C. Waefeso 6:14 Kujifunga ukweli viunoni.

Ombi: *Uniongoze katika kweli yako, na kunifundisha. Maana Wewe ndiwe Mungu wa wokovu wangu, nakungoja wewe mchana kutwa.* —Zaburi 25:5

UKWELI NI NINI?

Nakala ya Kuandamana na Mafunzo ya Biblia

"UKWELI NI NINI?" Hilo ndilo swalii ambalo Pilato alimuuliza Yesu alipokuwa akifanyiwa kesi mbele yake. Swalii hilo lingali limesimama wima hadi siku zetu ambako watu wanatafuta kote ulimwenguni ili wapate majibu ya maisha haya na shida zake. Wahubiri wengi wa injili, makanisa, na watu wanaofuata thiolojia tofauti tofauti, na hata wanafalsafa wamedai kwamba "wanao ukweli." Je, kwawezaje kuwa na mawazo tofauti yenye mgongano na hata maoni tofauti ambayo yote husemwa kuwa ni ukweli?

UKWELI NI MMOJA TU

Jambo la uhakika ni kwamba ukweli kamili ni mmoja tu.

Ukweli huo hupatikana ndani ya Yesu Kristo peke yake. Yesu ni kweli. Neno la Mungu ilifanyika mwili na kudumu kati yetu ili kutupatia mwangaza, kudhihirisha dhambi, kuonyesha na kufundisha ukweli wa utakatifu na ukombozi kutoka dhambini, na pia kuleta uwezekano wa mtu kuwa na amani nafsini mwake katika uhusiano wake na Mungu kama Baba yake.

UKWELI HAUBADILIKI

Mungu alimtuma Roho wake ili kuongoza watu kibinasi katika njia ya ukweli. Ukweli ni zaidi ya maoni, zaidi ya mambo ambayo mtu amepitia, zaidi ya historia ya kanisa, zaidi ya tamaduni, zaidi ya tabaka, na zaidi ya semi za kweli za dini. Ukweli wa Mungu haubadiliki toka kizazi kimoja hadi kingine lakini ungali ni wa kutegemewa na unatoa jawabu kuhusu maisha ya milele katika ulimwengu huu wa sasa ambao ni mwovu. Falsafa na vikundi vyta kikanisa huja na kwenda lakini ukweli ni wa milele na hubadiliki. Ukweli hautegemei mawazo yetu au hali zetu za kibinasi. Neno la Mungu linaweza kutumika na linafaa kwa watu wote wa mataifa mbali mbali. Kwa kweli Roho wa Mungu hawaongozi watu kinyume na ukweli wa Neno lake.

UKWELI HUWEKA HURU

Ukweli huleta mwangaza na kufanya mtu kuwa huru. Mafundisho na dini za mwanadamu humletea mtu utumwa na hali ya kuchanganyikiwa. Hata ikiwa kuna mafundisho tofauti ya kidini yenye mgongano na hata makanisa tofauti tofauti jambo hili haliondoi uhakika kwamba kungali kuna



ukweli. Ukweli huo hupatikana ndani ya Kristo na umenakiliwa katika Biblia, na pia kupewa uhakika na Roho Mtakatifu. Ukweli huo hauwezi kuongezewa au kupunguzwa kuitia kwa uamuzi wa kura ya wachungaji au tangazo kutoka kwa askofu au kiongozi wa kidini. Neno la Mungu husimama wima likiwa peke yake kama ukweli. Maandiko ya Neno la Mungu yamekamilika. Watu wa Mungu walio wa kweli hutukuza na kuheshimu neno la Mungu kama ukweli ambao hukanyangia chini mafundisho yote ya kibinadamu.

NENO LIKAFANYIKA MWILI

Kuna watu wengi ambao hujitangaza kuwa ni wafuasi wa Kristo lakini kukana ukweli wa matumizi ya Neno lake maishani mwao. Hata kuna wengine ambao hujaribu kutofautisha kati ya Yesu na mafundisho ya Biblia. Lakini ukweli ni kwamba Yesu na Neno Lake ni kitu kimoja. Mtu ye yoyote anayekataa sehemu yoyote ya mafundisho ya Agano Jipya huwa anamkataa Kristo mwenyewe.

KATAENI MANABII WA UWONGO

Katika kanisa la kwanza kulikuwa na waalimu wa uwongo na hata kanisa la sasa lingali hivyo kwa sababu lina wahudumu wa injili ambao wanamkiri Kristo lakini hawafundishi ukweli kamili. Wao hufundisha ukweli ambao wao wenye wamekira na ambao hutukuza vitendo vya dhambi na vya kufurahisha mwili ili kuwavutia umati mkubwa wa watu. Kusema kweli udanganyifu mkubwa hupatikana katika makanisa na kuitia wahudumu wa injili ambao hufundisha kiwango kikubwa cha ukweli lakini hawafundishi ukweli wote. Ni rahisi zaidi mtu kutambua mtu aliyepeota kabisa na kuwa mbali na ukweli kuliko kutambua ukweli ambao umechanganyishwa na upotovu. Basi ni muhimu kwamba tusiongezee au kuondoa kutoka kwa kile ambacho kimeandikwa katika Neno la Mungu.

UKWELI UMETENGANISHWA NA UDINI

Katika siku hizi za mwisho watu wengi wanaacha ukweli wa Neno la Mungu lakini wanadumisha ushahidi wa utakatifu

(Inaendelea kutoka ukurasa 6)

(Endelea kutoka ukurasa 5)

wa nje. Lakini maandiko yanafundisha kwamba watu wa kweli wa Mungu hujitenga kutokana na vikundi kama hivyo vya kibinadamu na wao huacha kuwa na ushirika na wahudumu wa injili wa aina hiyo. Mbingu inaita wale ambao ni waaminifu na watakatifu, lakini jehanamu yangoja wale ambao wanakataa ukweli wote.

ROHO MTAKATIFU NDIYE USHUHUDA KWA ULIMWENGU

Ni jambo la lazima kwa kila mtoto wa Mungu kujazwa Roho Mtakatifu na kujifunza Neno la Mungu. Roho atakuwa mwaminifu kwa kila mtu ambaye ni mkweli na ambaye anatafuta ukweli kwa dhati. Watu wako katika viwango tofauti katika uelewaji wao wa ukweli. Ndiposa uwajibikaji ni wa kiwango tofauti kwa watu tofauti. Shida hutokea wakati mtu binafsi anapuuza sauti ya Roho na ya Neno lililoandikwa. Hapo ndipo hadaa huingia na watu kuanza kushawishika kuhusu

maoni yao ya kibinafsi ya ukweli. Lakini mtu akiwa mkweli hii haimfanyi kukubalika machoni pake Mungu. Ni pale ambapo mtu mkweli anaingiza ukweli wa Mungu ndani yake ndipo mwanadamu anawezeshwa kuishi maisha yanayokubalika na Mungu. Basi wewe kuwa mwaaminifu kwa Neno la Mungu na ujue kwamba Roho wa Mungu kamwe hatawahi kuongoza mtu kutenda jambo ambalo ni kinyume na Neno la Mungu.

JE, WEWE WAISHI KULINGANA NA UKWELI?

Kanisa la Mungu ni ushirika wa kibinafsi na wa pamoja wa watu ambao wanaruhusu ukweli kufanya kazi katika kila fani ya maisha yao. Sayuni, ambayo ni Kanisa la Mungu, ni mji ambao unahitaji kuwa wa ukweli. Basi cha muhimu silo jina la kanisa bali ni kufanyishwa kazi kwa ukweli ambao uko hai. Basi ni ombi langu kwamba mwangaza wa ukweli huu utang'aa zaidi kote maishani mwako. ■



Iweni Watendaji

*"Lakini iweni watendaji wa neno,
wala si wasikiaji tu,
halis mkijidanganya nafsi zenu.
Kwa sababu mtu akiwa ni msikiaji wa neno tu, wala
si mtendaji,
mtu huyo ni kama mtu anayejiangalia uso wake kati-
ka kioo.
Maana huijiangalia, kisha huenda zake,
mara akasahau jinsi alivyo.
Lakini alyeitazama sheria kamilifu iliyo ya uhuru,
na kuka humo, asiwe msikiaji msahauifu,
balis mtendaji wa kazi,
huyo atakuwa heri katika kutenda kwake."*

Yakobo 1:22-25

SWALI

na

JIBU




(Nakala hii imenekuliwa kwa kimuhstasari kutoka kwa maandishi ya hayati Bro. Ostis Wilson Jr.)

Swali: Mara nyingi tumesikia msemo unaosema haijalishi watu wanaamini nini mradi wao wanaamini hivyo kwa dhati. Je, jambo hilo ni la kweli?

Jibu: LA HASHA! Inawezekana watu kuwa wamepotea na waamini wanayoamini kwa dhati kama ambavyo wanaweza kuamini ukweli kwa dhati. Neno la Mungu linasema, "kwa kuwa Mungu amewachagua tangu mwanzo mpare wokovu, katika kutakaswa na Roho, na kuiamini kweli" (2 Wathesalonike 2:13). Hapa twaona kwamba "kuamini kweli" ni sehemu muhimu ya njia na mpango wa Mungu wa sisi kupata wokovu. Nayo 2 Timotheo 4:3-4 inasema, "Maana utakuja wakati watakapoyakataa mafundisho yenyeye uzima; ila kwa kuzifua nia zao wenye kwa watajipatia waalimu makundi makundi, kwa kuwa wana masikio ya utafiti; nao watajipusha wasisikie yaliyo kweli, na kuzigeukia hadithi za uongo." Baadhi ya watu hawa wana udhati mwangi ndani yao na wamejitelea kwa nguvu kwa yale ambayo wameamini kama jinsi ambavyo wale ambao wanaamini ukweli wamejitelea.

Mtume Paulo alisema katika Wagalatia 1:8-9, "Lakini ijapokuwa sisi au malaika wa mbinguni atawahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa hiyo tuliyowahubiri, na alaaniwe. Kama tulivyotangulia kusema, na sasa, nasema tena, mtu awaye yote akiwahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa

hiyo mliyopokea, na alaaniwe." Hapa mtume Paulo ametumia lugha kali na haijalishi tunatumia tafsiri gani ukweli ni kwamba andiko hilo linafundisha kwamba kile ambacho Mkristo anaamini kinahitaji sio tu kulingana na ukweli bali pia msingi wake unahitaji kuwa wa ukweli. Imani pia inahitaji kulindwa kuititia kwa mipaka ya ukweli ambayo haikiuki ukweli na ambayo haikubali mafundisho ya uwongo.



Katika 2 Wakorintho 1:12 mtume Paulo ananena kuhusu "... utakatifu na weupe wa moyo ..." wake. Mtu anaweza kuwa na weupe ndani yake katika imani au mradi wowote ambao anauamini; lakini ni weupe tu wa kiungu ambao ndio utamletea wokovu na kumwekea misingi mizuri ndani yake Mungu.

Mtume Paulo mwenye aliwa mfano wa ajabu kuhusiana na swala hili. Katika Matendo ya Mitume 26:9-10 yeye anasema, "Kweli, mimi mwenye nalionia ndani ya nafsi yangu kwamba yanipasa kutenda mambo mengi yaliyopingamana na jina lake Yesu

Mnazareti." Hata ingawa alikuwa na dhati na weupe ndani yake yeye mwenye aliwa angalikosa kupata wokovu kama hangenyekeea kwake Kristo na kumwamini wakati walipokutana ana kwa ana hapa katika njia ya kuelekea Dameski.

Mimi nadhani kwamba Mtume Paulo hakuwa na udhati na weupe ndani yake kwa ajili ya ukweli na kwa ajili ya imani yake ya Kikristo kuliko jinsi alivyokuwa na udhati na weupe ndani yake kwa ajili ya dini ya Kiyahudi na tamaduni za mababu zake. Bila shaka kuna baadhi ya watu ambao wana udhati na weupe mwangi ndani yao na hata kujitolea kwa kiwango kikubwa na kujinyima kwa mambo ambayo yamepotoka kutoka kwa ukweli na ambayo huwa yamekana baadhi ya mambo ya kimsingi ya wokovu, kama jinsi ambavyo Wakristo wamejitelea kwa Kristo na kwa ukweli. Basi kumbuka kwamba jambo muhimu sio tu udhati na weupe kwa yale unayoamini bali hasa ni udhati na weupe kwa mambo ya kiungu.

Tunahitaji kuzingatia pia kwamba kama imani ya aina yote ya mtu yeote ingekuwa halali na ya kukubalika mradi tu kwambe awe na udhati na weupe ndani yake jambo hili lingehalisha viwango tofauti vya maisha lakini Mungu anacho kiwango kimoja tu na Yeye anawaita watu wote kuja kwenye kiwango hicho. Waefeso 4:5 inasema "... kuna imani moja, ..." Basi Mungu anawaita waumini wote kufikia "umoja wa Imani" na ametoa uwezo wa kutuleta sisi sote kufikia hayo ikiwa sote tutaamini mafundisho ambayo yana uaminifu kwa Neno la Mungu. ■

Jiandikishe ili Upate Nakala Yako!

RAHISI. HARAKA.YA KUFAA. BILA MALIPO.

Tutembelee katika tovuti yetu ya www.thegospeltruth.org ili ujiandikishe kupata nakala yako ya kielektroni-ki bila malipo. Papo hapo utapata barua pepe ambayo itakujulisha na kukuruhusu kupata kila nakala mpya. Basi jiandikishe leo kupata nakala yako na ushiriki mambo haya na watu wengine.



BORA NINYI

Anwani

The Gospel Truth
P. O. Box 2042
Nixa, MO 65714
USA
Email
editor@thegospeltruth.org

UTAKATIFU KWA BWANA

"Je! Mashomoro watano hawauzwi kwa senti mbili? Wala hasahauliwi hata mmojawapo mbele za Mungu. Lakini hata nywele za vichwa vyenu zimehesabiwa zote. Msigope basi, bora ninyi kuliko mashomoro wengi" (Luka 12:6-7).

Katika wakati wa Kristo mashomoro wawili wangenunuliwa kwa senti moja. Nao mashomoro wanne wangenunuliwa kwa senti mbili, nayo ya tano kuongezewa kama nyongeza ya wafanya biashara ili kuwavutia wanunuaji kununua mashomoro wanne. Nunua wanne upate shomoro wa tano bila malipo! Senti moja ilikuwa thuluthi moja kwa kumi na sita (1/16) ya malipo ambayo mfanyi kazi wa sehemu za mashambani angepata kwa siku moja. Basi mashomoro yalikuwa ndege wa kawaida na gharama yake ilikuwa hafifu kabisa.

Basi Yesu anaonyesha jinsi Mungu anavyowajali watu kibinasi kwa kufanua jinsi ambayo Yeye hapuuzi hata kitu cha kawaida na cha gharama ya chini kama shomoro mmoja – maa-nake ndege wa tano. Mungu huwekea thamani mambo ambayo watu wengine huona kwamba hayana thamani. Basi hii ni kusema Mungu anapenda na kumjali kila mwanadamu kwa kiwango kipi! Yeye huona zaidi ya umati na kumthamini kila mtu binasi. Mungu hushughulishwa na kila swala maishani mwa mwanadamu: kila wazo lake, kila hisia, vile anavyojihisi, na kusema kweli kila hali aliyo nayo maishani mwake. ■

